



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

WAKALA WA HUDUMA YA UNUNUZI SERIKALINI



Anuani: "GPSA" DSM
Mtaa wa Bohari/Barabara ya Nyerere – Keko Mwangi
Simu: Na. 022-2866071/2861617
Simu Na. 2118869 – C/Forwarding
Barua pepe: ceo@gpsa.go.tz
Tovuti: www.gpsa.go.tz
(Mawasiliano yote ya kiofisi
yaandikwe kwa Mtendaji Mkuu na
siyo kwa mtu binafsi:-

S.L.P 9150,
DAR ES SALAAM

Unapojibu tafadhali taja:

30 Juni, 2023

Kumb. Na. AB.10/422 /01.F/168

Wazabuni wa Mikataba Maalum (Framework Agreement)

Vifaa na Huduma Mtambuka (CUIS)

Mwaka wa Fedha 2022/2023

TANZANIA BARA

YAH: KUONGEZA MUDA WA MIEZI MITATU WA MIKATABA MAALUM (FA) YA VIFAA NA HUDUMA MTAMBUKA YA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Tafadhali husika na kichwa cha habari tajwa hapo juu.

2. Zoezi la kuwapata wazabuni wa Vifaa na Huduma Mtambuka wa mwaka wa fedha 2023/2024 halijafanyika hadi sasa kama ilivyozoeleka kufuatia ujenzi wa mfumo mpya wa kielektroniki wa ununuzi wa umma (**NeST**) ambao utatumika kuwapata wazabuni.
3. Kwa kuwa ujenzi wa Moduli ya "Framework Agreement" kwenye mfumo wa NeST bado haujakamilika na kufuatia ukomo wa mikataba ya Vifaa na Huduma Mtambuka ya mwaka 2022/2023 kumalizika tarehe 30 Juni, 2023 kwenye mfumo wa TANePS, tunapenda kuwafahamisha kwamba, **tumeongeza muda wa miezi mitatu (3) kuanzia tarehe 01 Julai hadi 30 Septemba, 2023 kwa Mikataba ya Vifaa na Huduma Mtambuka (CUIS)** iliyokuwa inaishia tarehe 30 Juni, 2023 kama matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma Kifungu Na. 77(3) ya mwaka 2011 na Kanuni Na. 111(1) za mwaka 2013 na Marekebisho ya mwaka 2016 yanavyoelekeza.
4. Hivyo basi mikataba hiyo itaendelea kutumika kwenye mfumo wa TANePS hadi tarehe 30 Septemba, 2023.
5. Asante kwa ushirikiano.


Prof. Geraldine A. Rasheli
AFISA MTENDAJI MKUU

- Nakala:** 1. Afisa Mtendaji Mkuu
Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA)
S. L. P. 2865
DODOMA
2. Taasisi Nunuzi za Serikali
TANZANIA BARA